**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

# TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 08/05/2024 KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA TATU MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

- Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Siha,
- Katibu Tawala-Mkoa wa Kilimanjaro,
- Mh. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Siha,
- Mhe. Makamu Mwenyekiti Halmashhauri ya Siha
- Waheshimiwa Madiwani,
- Ndugu Mkurugenzi  Mtendaji (Katibu wa Baraza),
- Wah Viongozi wa Madhehebu ya  Dini,
- Wageni Waalikwa,
- Ndugu Wataalamu,
- Waandishi wa Habari,
- Wananchi wa Wilaya ya Siha,
- Mabibi na Mabwana,

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA…… KAZI IENDELEE**

Wah. Madiwani,Viongozi mbalimbali na Wananchi, Nawasalimu wote kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Kipekee namshukuru Mungu kwa uzima na Afya ambao Mungu ameendelea kutupatia sisi Viongozi pamoja na Watumishi na Wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Siha, naomba tutumie uzima na afya tulizonazo katika kuwatumikia Wananchi wa Wilaya ya Siha ili wapate huduma zote stahiki bila upendeleo wala ubaguzi wowote.

Kwanza kabisa kwa niaba ya Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Siha napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mhe.Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoingoza Nchi yetu kwa weledi mkubwa na kufanya Tanzania kuwa nchi ya pekee inayokimbiliwa na watu wa mataifa mbalimbali kutoka Bara la Afrika pamoja na Mabara mengine.

Pia napenda kumshukuru na kumpongeza Jembe letu Siha Mhe. **Dkt Godwin Mollell** Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha kwa jinsi anavyotuwakilisha vema katika Bunge hususani kutupambania kupata fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika Jimbo la Siha

Napenda pia kumshukuru Mkuu wetu wa Wilaya kwa jinsi anavyotuongoza na kutushauri vizuri kwani amekuwa anatufundisha nidhamu ya muda na kuwa watu wa kukomboa wakati katika utendaji kazi

**Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi**

Vilevile naomba kuwashukuru Viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Siha wakiongozwa na Mwenyekiti wetu **Mhe. Wilfred Mosi** (Babalao) kwa jinsi anavyoongoza chama kwa hekima na kutufanya tuwe wamoja wakati wote, nasi kama Waheshimiwa Madiwani tunaahidi kuwa tutaendelea kufanya kazi kwa bidi na maarifa na kuhakikisha kuwa Chama cha Mapinduzi kinapata ushindi mkubwa katika uchaguzi wa Serikali za **mitaa mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu mwaka 2025**

**Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,**

Katika taarifa yangu kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/2024 yapo mambo mbalimbali nimeyajumuisha kwa lengo la kuweka msisitizo na kufahamisha umma mambo yaliyofanyika na kutekelezwa na Halmashauri kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

I. **Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri,**

Katika Kipindi cha robo ya tatu nimepata taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani umefikia zaidi ya asilimia 93 na kuonesha kuwa ipo kazi kubwa imefanywa na Wataalam wetu wa Halmashauri wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji.kwa hili napenda kuwapongeza Wah. Madiwani wote kwa ushauri na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani hali iliyofanya ukusanyaji wa mapato kufikia zaidi ya asilimia 93 kabla ya kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2023/2024, Naomba kutoa wito kwa Mkurugenzi Mtendaji na Wataalam wake kuendelea kuweka nguvu zaidi ya ufuatiliaji wa mapato halali ya

Halmashauri kwa kuzingatia sheria,Kanuni na Taratibu na Nchi zilizopo na kamwe tusikubali mapato kupotea kwa namna yoyote ile.

Naomba niendelee kuhimiza na kusisitiza kuwa sisi kama wawakilishi wa Wananchi hatutakuwa na msamaha kwa mtumishi yeyote atakayethubutu kuhujumu au kutumia fedha za Makusanyo ya Halmashauri hususani fedha zinazokusanywa kwa kutumia mashine za kieletroniki (POS) bila kufuata utaratibu wa Serikali,bali nahimiza kila mtumishi kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba wake wa ajira na kuendelea kufanya kazi za utumishi wa umma kwa uadilifu na weledi.

## II. Utunzaji wa Mazingira na Usafi

**Wah. Madiwani,Viongozi na Wananchi:**

Kama tunavyojua kipindi hiki ni kipindi cha mvua nyingi naomba kutoa wito kwa wananchi kupanda miti mingi katika maeneo ya mashamba na majumbani hususani miti ya matunda na mbao.

Natoa rai kwa Mkurugenzi Mtendaji na Wataalam wako endeleeni kusimamia agizo la Serikali la kila jumamosi ya mwisho wa mwezi kushiriki katika usafi wa mazingira kwani naona jambo hili limelegalega katika baadhi ya maeneo jambo ambalo linaweza kuleta hatari ya kutokea magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu. Sisi kama viongozi tupo tayari katika kuendelea kutekeleza agizo hilo muhimu kinachotakiwa wekeni utaratibu wa kuzunguka kila Kata katika eneo likakalopendekezwa.

## III. Athari za Mvua ya Masika

**Wah. Madiwani,Viongozi na Wananchi**

Wilaya yetu ya Siha katika kipindi cha mvua za masika tumepata mvua nyingi ambazo mvua hizi zimeleta athari kubwa katika mashamba, mazao,miundombinu ya barabara ,majengo ya shule za msingi na sekondari na maeneo mengine ya jamii kama vile ofisi za Kata na Vijiji pamoja na maeneo ya Magulio.

Ukweli ni kwamba Athari za mvua hizi ni kubwa katika maeneo mengi ya Wilaya yetu hususani barabara za vijijini zimeharibika mno na kusababisha usumbufu kwa wananchi kushindwa kusafiri na kusafirisha mazao ya kilimo na biashara. Tunaomba Serikali itusaidia kukarabati miundombinu ya barabara zilizoharibika vibaya katika maeneo mbalimbali ya Wilaya yetu ya Siha.

Pamoja na uharibifu wa miundombinu pia baadhi ya mashamba yamejaa maji na kuharibu mazao ya wakulima na hivyo kufanya baadhi ya wananchi watakosa chakula cha kutosha na hivyo kuwa na uhitaji wa chakula kwa baadhi ya watu katika maeneo mbalimbali ya Wilaya yetu.

## IV. Uwajibikaji kazini kwa Watumishi wa Halmashauri

Kipekee napenda kuwapongeza Watumishi wote wa Halmashauri yetu kwa jinsi wanavyoendelea kutoa huduma bora kwa Wananchi na wakazi wa Wilaya ya Siha. Naomba utendaji huu wa kazi kwa watumishi uendelee kwa kuzingatia miongozo na sheria za utumishi wa Umma ili kumsaidia

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano** wa Tanzania katika dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha kuwa nchi inapata maendeleo ya haraka katika Nyanja za kiutamaduni,kisiasa,kiuchumi na katika ustawi wa jamii endelevu.

V. **Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru mwaka 2024**

**Wah. Madiwani,Viongozi na Wananchi:**

Napenda kuwapongeza na kuwashukuru Viongozi na Wananchi wote wa Wilaya ya Siha kwa jinsi mlivyoshiriki katika mapokezi ya Mwenge wa Uhuru **tarehe 4 Aprili,2024.** Mwenge wa Uhuru ulipokuwa katika Wilaya yetu umepita salama na mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu **GODFREY ELIAKIMU MNZAVA** ametoa pongezi nyingi kwa Wilaya yetu kwa jinsi tulivyoonesha ushirikiano mkubwa katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2024. Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru mwaka 2024:"***TUNZA MAZINGIRA NA SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA UJENZI WA TAIFA ENDELEVU"***

**Wah. Madiwani,Viongozi na Wananchi**

Pia katika tukio la maadhimisho ya Muungano napenda kuwapongeza Wananchi wa Wilaya ya Siha na Viongozi kwa jinsi mlivyoshiriki katika maadhimisho ya **miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo** Kiwilaya yaliyofanyika Kata ya Sanya Juu na mgeni rasmi alikuwa mkuu wetu wa Wilaya ya Siha Mhe.Dkt.Christopher Timbuka.

Naomba ushirikiano kama huu uendelee katika sherehe zote za kitaifa kwani mshikamano ndiyo nguzo yetu sisi Watanzania.

Kauli mbiu ya Muungano mwaka 2024: **MIAKA 60 YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUMESHIKAMANA NA TUMEIMARIKA KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU**

Kabla sijafika mwisho wa taarifa yangu naomba kutoa shukrani za dhati kwa niaba ya Baraza la Madiwani kwa Ofisi ya Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro kwa jinsi anavyosimamia vema Halmashauri yetu na wakati wote amekuwa akitushauri na kutuongoza vema

Aidha, Naomba niwashukuru tena Wah. Madiwani,Viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya kipekee Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Siha kwa jinsi mnavyofanya kazi kwa bidi na weledi mkubwa wa kuisimamia Halmashauri yetu.

Vilevile ,Nawashukuru Wananchi na Wakazi wa Wilaya ya Siha kwa usikivu wenu mkubwa mlionesha tangu mwanzo wa taarifa yangu hadi sasa ninapohitinisha taarifa yangu, naomba usikivu na utulivu huu uendelee hadi mwisho wa Mkutano wetu.

**Mungu ibariki Tanzania,Mungu ibariki Wilaya yetu ya Siha**

Asanteni sana kwa kunisikiliza

**Imetolewa na:**

**Mhe. Duncan B. Urassa**
Mwenyekiti wa Halmashauri (W) **SIHA**
**Tarehe 08/5/2024**